



**CDSC**

CENTRAL DEPOSITORY &  
SETTLEMENT CORPORATION LIMITED

HATI KUONDOLEWA

**M**K**M**

(Maswali ya kila mara)



**Salama, Haraka, Rahisi...**

1. **Je, maana ya Hati kuondolewa ni nini?**  
Hati kuondolewa ni hatua ya pili baada ya hisa kuhifadhiwa kwa njia ya elektroniki. Tarehe ya Hati kuondolewa itakuwa siku ya mwisho kwa hati ya hisa kutumika kama ushahidi wa umiliki wa hisa za shirika lolote linaloorodheshwa katika soko la hisa la Nairobi (NSE). Ushahidi wa umiliki utakuwa kupitia njia ya CDS, ikiwa ni mradi unaoendeshwa na CDSC
2. **Je, baada ya Hati kuondolewa dhamana ya hisa itakuwa nini?**  
Ni rekodi iliyowekwa kwa mujibu ya shirika la CDSC fungu la 24 ya sheria na kanuni za Central depositories , ambapo hati ya hisa haitatambulika kama ushahidi wa umiliki kuambatana na sheria na kanuni za kampuni sura ya 486, au baada ya tarehe ya Hati kuondolewa.
3. **Je, tarehe ya Hati ya kuondolewa ni lini?**  
Ni tarehe iliyowekwa na CDSC kwa mujibu ya fungu la 24 kuwa siku ya mwisho ya kutambua hati ya hisa kuwa ushahidi wa umiliki kwa mujibu wa sheria na kanuni za kampuni fungu la 486. Tarehe hiyo ni Novemba 30, 2012.
4. **Je, Hati kuondolewa kutasababisha nini?**  
Kwa wakati huu hisa zinaweza kutolewa kutoka kwa akaunti ya CDSC na kuwekwa kama hati. Walakini baada ya tarehe ya Hati kuondolewa (**30 Novemba 2012**) haitawezekana kutoa hisa kutoka CDSC kwa kuwa sheria hairuhusu matumizi ya hati.
5. **Je, baada ya Hati kuondolewa, jukumu la msajili wa hisa itakuwa nini?**  
Watakaohusika hawataweza kutoa hati za hisa kwa mwenyehisa aidha iwe ni kwa sababu ya kununua hisa, toleo la hisa za ziada, toleo la hisa hakiki, au ugawaji wa hisa. Hizi zote zitatolewa kwa njia ya elektroniki.
6. **Je, nitahitajika kufanya nini nikiwa mwenyehisa kama tayari nimekwisha weka hisa zangu kwenye akaunti ya CDSC?**  
Hautahitajika kuchukua hatua zozote kwa msajili wa Hati kuondolewa.
7. **Je, kuna manufaa ya Hati kuondolewa?**
  - Hati za hisa hazitapotea kwa sababu zitawekwa kwa njia ya elektroniki.
  - Itakuwa rahisi na haraka kuhamisha au kuuza hisa.
  - Hati yako ya hisa haitaharibika kwa kuwa zitawekwa kwa njia ya elektroniki.
  - Utaweza pia kuweka hati ya hisa kama kumbukumbu.
  - Gharama ya kutoa hisa mpya itapungua.
10. **Je, ni nini itafanyika kwa hisa zangu baada ya tarehe 30 Novemba 2012?**  
Baada ya tarehe ya Hati kuondolewa, msajili wako atafungua akaunti ambapo hisa zote ambazo hazijahifadhiwa kwa njia ya elektroniki zitawekwa kwa niaba yako na anayehusika.
11. **Je, na nikitaka kupata hisa zangu ambazo nimewekwa kwa niaba na anayehusika?**  
Ikiwa utahitaji hisa zako kwa minajili ya kuuza, au kuhamisha itakubidi kujitambulisha kwa msajili anayehusika na baadaye hisa zako zitahamishwa kwenye akaunti yako ya CDS utakayofungua
12. **Je, nitawezaje kufuatilia hisa zangu?**  
CDSC itatatumia kwako stementi kila mwezi kama akaunti yako itakuwa na shughuli nyingi ,la sivyo utapokea stementi mara moja kila mwaka. Walakini ikiwa utahitaji kuangalia/chapisha nakala ya stementi yako unaweza kufanya hivyo kupitia wavuti yetu: [www.cdsckenya.com](http://www.cdsckenya.com). Unaweza pia kujisajili ili uweze kupata huduma kupitia simu ya rununu ambapo utaweza kupata arafa fupi kila mara kuna shughuli katika akaunti yako ,kwa mfano ujumbe wa kibiashara, mauzo au ununuzi na kadhalika, kwa ada kidogo ya Shilingi(k) 10 kwa kila arafa. Ili kujisajili tuma neno "register" kwa nambari **2372** na ufuate maagizo.

#### **Kwa maelezo zaidi tembelea sisi ,**

Nation Centre ghorofa ya 10,  
Kimathi street,  
P.O.BOX 3464 00100  
Nairobi

Simu: +2540202912000/2229407  
Rununu: 0724256130/0733222033  
Wavuti: [helpdesk@cdsckenya.com](mailto:helpdesk@cdsckenya.com).